



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA NYANG'HWALE



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb.NA.AC/12/214/83

03/05/2024

TANGAZO LA KAZI YA MKATABA

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale kwa kuzingatia Kibali cha Ajira za Mkataba wa mwaka mmoja cha tarehe **02/04/2024** chenye **Kumb.Na. FA.97/228/02”A”/136** kutoka kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, anakaribisha maombi ya kazi kwa Watanzania wenyе sifa na uwezo wa kujaza nafasi ya kazi ifuatayo:

1.0 MHANDISI II (UJENZI) - Nafasi 01

1.0.1 KAZI NA MAJUKUMU.

- i. Atafanya kazi chini ya uangalizi wa Mhandisi aliyesajiliwa na Bodi ya Usajili ya Wahandisi (Professional Engineer) ili kupata uzoefu unaotakiwa.
- ii Kufanya ukaguzi wa barabara, madaraja na majengo mbalimbali.
- iii.Kuchunguza vyanzo vya ajali mbalimbali zinazohusiana na majengo.
- iv.Kufuatilia utekelezaji wa Sheria na Kanuni za ujenzi wa barabara na majengo.
- v.Kutayarisha bajeti ya mwaka ya ujenzi na matengenezo ya barabara, madaraja na majengo.
- vi.Kusimamia na kuratibu kazi za barabara / madaraja na majengo zinazotolewa na Makandarasi; na
- vii.Kufanya kazi zingine atakazopangiwa na Msimamizi wake wa kazi.

1.0.2 SIFA ZA MWOMBAJI

Kuajiriwa mhitimu wa kidato cha Nne/Sita aliofuzu mafunzo ya Shahada / Stashahada ya Juu katika fani ya Uhandisi Ujenzi kutoka katika vyuo vinavyotambuliwa na Serikali na wawe wamesajiliwa na Bodi ya Usajili ya Wahandisi (ERB).

1.0 .3 Ngazi ya Mshahara TGS E.

MASHARTI YA JUMLA.

- i. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na wenye umri usiozidi miaka 45 isipokuwa kwa wale tu walioko kazini serikalini;
- ii. **Waombaji wenyе ulemavu wanahamasishwa kutuma maombi na wanapaswa kuainisha kwenye mfumo wa kuombea ajira ulemavu walionao kwa ajili ya taarifa kwa Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma;**
- iii. Waombaji wote waambatishe cheti cha kuzaliwa kilichothibitishwa na Mwanasheria/Wakili.
- iv. Waombaji ambao tayari ni watumishi wa Umma na wamejipatia sifa za kuingilia katika kada tofauti na walizonazo, wapitishe barua zao za maombi ya nafasi za kazi kwa Waajiri wao na Waajiri wajiridhishe ipasavyo.
- v. Waombaji waambatishe maelezo binafsi yanayoitosheleza (Detailed C.V) yenye anwani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (referees) watatu wa kuaminika.
- vi. Maombi yote yaambatane na vyeti vya taaluma, maelezo, nakala za vyeti vilivyothibitishwa na Mwanasheria/Wakili ambavyo ni vyeti vya kuzaliwa, kidato cha Nne, kidato cha Sita kwa wale waliofikia kiwango hicho, na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika.

Postgraduate/Degree/Advanced Diploma/Diploma/Certificates. - Cheti cha mtihani wa kidato cha IV na VI - Computer Certificate - Vyeti vya kitaaluma (Professional certificates from respective boards)

- vii. “Testimonials”, “Provisional Results”, “Statement of results”, hati matokeo za kidato cha nne na sita (FORM IV AND FORM VI RESULTS SLIPS)

HAVITAKUBALIWA.

- viii. **Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika (TCU, NECTA na NACTE).**
- ix. Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wana kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.
- x. Waombaji kazi ambao tayari ni waajiriwa katika nafasi za kuingilia walioko katika Utumishi wa umma wasiombe na wanatakiwa kuzingatia maelekezo **yaliyo katika Waraka Na CAC. 45/257/01/D/140 wa tarehe 30 Novemba, 2010.**
- xi. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.
- xii. Waombaji wote waambatishe nakala ya kitambulisho cha Taifa (NIDA) -Kwa ambao hawana vitambulisho,namba za NIDA ziandike kwenye maelezo binafsi (CV)
- xiii. **Mtumishi atakayeajiriwa atapewa Mkataba wa mwaka mmoja (1). Anaweza kuongezewa mwaka mmoja (1) mwingine kutegemea na utendaji wa kazi wake (Renewable once)**
- xiv. Maombi yote yatumwe kwa njia ya Posta kwa kutumia anuani ifuatavyo:

**MKURUGENZI MTENDAJI(W)
HALMASHAURI YA WILAYA YA NYANG'HWALE,
S.L.P 352,
NYANG'HWALE.**

MWISHO WA KUPOKEA MAOMBI YA KAZI NI TAREHE 16 MEI, 2024 SAA 9:30 ALASIRI

NB: Tangazo hili linapatikana katika Tovuti ya Halmashauri ambayo ni www.nyanghwale.go.tz mbao za matangazo Ofisi za Kata pamoja na Tovuti ya Sekretarieti ya Ajira www.ajira.go.tz.

Limetolewa na:

Husna Toni
**MKURUGENZI MTENDAJI (W)
NYANG'HWALE**

